


# **DIRA —YA— KUJIAJIRI**

- Maana ya kujiajiri na faida zake**
- Vikwazo vya kutojiajiri na namna ya kuvikabili**
- Misingi ya kuzingatia katika kujiajiri**
- Changamoto baada ya kujiajiri na utatuzi wake**
- Miradi ambayo mtu anaweza kujiajiri**



**Hamza Juskas**

## KUHUSU MWANDISHI

Kitabu hiki kimeandikwa na **Hamza S. Juskas**, ambaye ni mwalimu na mtaalamu wa sayansi ya viumbe hai (biology), kilimo na ufügaji (agriculture), mwandishi na mjasiriamali.

---

**Simu:** 0789589534

**WhatsApp:** 0622202879

**Baruapepe:** juskas08@gmail.com

---

**Hakimiliki©Hamza Juskas**

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kupiga chapa, kukodisha, kunakili, kutafsiri katika lugha nyingine au matumizi ya namna yoyote bila idhini ya mwandishi.

*Toleo la kwanza Julai 2021*

*Mwl. Juskas*

## UTANGULIZI

**“DIRA YA KUJIAJIRI”** ni kitabu nilichoandika kwa lengo la kutoa mwongozo mwelesi utakaomwezesha kila mwenye nia ya kujiajiri akiwemo mjasiriamali, mhitimu au hata mwajiriwa ili ajiajiri katika shughuli yoyote anayoipenda ili aweze kuijingizia kipato na kujiimarisha Kiuchumi.

**Wahitimu** wengi wanashindwa kujiajiri kwa kukosa mwongozo mzuri utakaowawezesha kujiajiri na wanabaki hawana ajira kwa kuwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya ajira rasmi serikalini na hata mashirika binafsi kutokana na kuwa na wasomi wengi wa ngazi mbalimbali za elimu.

Kupitia kitabu hiki **wajasiriamali** watapata maarifa na mwongozo ili waweze kujiajiri katika Miradi au Maeneo mbalimbali wanayoyapenda na kuijingizia kipato hatimaye kujiimarisha kiuchumi.

**Waajiriwa** wakisoma kitabu hiki watapata mwongozo wa namna kujiajiri katika kazi ya ziada wanazozipenda ili waweze kuijingizia kipato na waweze kukidhi mahitaji yao na hata kufikia kuweka akiba. Waajiriwa wengi wamekuwa wakiishi kwa kutegemea mshahara ambao mara nyingi hakuna akiba baada ya matumizi ya mshahara, hivyo wamekuwa wakiishi maisha ya kujirudia rudia na wakijipa matumaini kwa kusema "nakula, naishi na kulala" basi inatosha, jambo ambalo linawafanya wasipige hatua ya kimaendeleo miaka mingi, wengine huishi kwa mikopo.

## YALIYOMO

<b>KUHUSU MWANDISHI .....</b>	<b>1</b>
<b>SEHEMU YA 1 .....</b>	<b>4</b>
MAANA AJIRA NA KUJIAJIRI.....	4
Ajira ni nini? .....	4
Kujiajiri ni nini? .....	9
<b>SEHEMU YA 2 .....</b>	<b>11</b>
FAIDA ZA KUJIAJIRI .....	11
<b>SEHEMU YA 3 .....</b>	<b>15</b>
VIKWAZO VINAJVYOWAFANYA WATU WASIJIAJIRI .....	15
<b>SEHEMU YA 4 .....</b>	<b>29</b>
MISINGI YA KUZINGATIA KATIKA KUANZISHA BIASHARA.....	29
<b>SEHEMU YA 5 .....</b>	<b>31</b>
CHANGAMOTO BAADA YA KUJIAJIRI .....	31
<b>SEHEMU YA 6 .....</b>	<b>36</b>
MIRADI AMBAYO MTU ANAWEZA KUJIAJIRI .....	36
Miradi 100 unayoweza kujiajiri .....	48

*Mwl. Juskas*

## **SEHEMU YA 1**

### **MAANA AJIRA NA KUJIAJIRI**

#### **Ajira ni nini?**

Ni mkataba maalumu ambao hufungwa baina ya mwajiri na mwajiriwa kwa malipo ya kipindi walichokubaliana. Kitu kikubwa kilichopo katika ajira ni kwamba mwajiri ananunua muda na maarifa ya mwajiriwa kwa makubaliano ya kumlipa mwajiriwa ujira kila baada ya muda fulani na mara nyingi mwezi ndio hutumika.

Kiasi cha malipo anayoyapata mwajiriwa kutoka kwa mwajiri wake kila mwisho wa mwezi au muda fulani waliokubaliana huitwa mshahara. Ujira huo unaweza kuwa kitu chochote cha thamani lakini mara nyingi pesa ndio inayotumika kama ujira.

Mwajiriwa anakuwa tayari kufanya kazi katika kampuni, ofisi, taasisi au shirika fulani kwa sababu anajua mwisho wa mwezi atapata mshahara